

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA CHALINZE
(Barua zote ziandikwe kwa Mkurugenzi Mtendaji)

Simu Na. 023 2440164
Nakishi. 023 2440338

E - MAIL:
dedchalinze@pwani.go.tz




Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji (W)
S.L.P. 65,
CHALINZE.

KUMB.NA.HWC/L.20/3/VOL.IV/80

Mkurugenzi Mtendaji
Kituo cha Taifa cha Uwekezaji
S.L.P 938

DAR ES SALAAM



YAH: VIWANJA NAMBA 18 HADI 33, KITALU "D" PINGO, CHALINZE MKOA WA PWANI

Ofisi yetu imepokea barua yenye Kumb. Na. DCG/0405/21/TZ ya tarehe 5 Mei 2021 toka Kampuni ya DATACOM HOLDINGS LIMITED ikiomba kutolea kwako ufafanuzi wa taarifa sahihi kuhusu umiliki wa viwanja tajwa hapo juu kwa Kampuni ya kigeni ya ATLAS BRICKS CO. LTD.

Kwa barua hii, tunapenda kukufahamisha kuwa, viwanja tajwa vimetokana na mgawanyo wa kilichokuwa kiwanja Namba 4, Kitalu _ Pingo, kilichokuwa kikimilikiwa kisheria na Kampuni ya DATACOM HOLDINGS LIMITED. Viwanja hivyo vilibuniwa kwa mchoro wa Mipangomiji uliosajiliwa kwa namba 52/CH/07/01108B tarehe 1 Juni 2018 na upimaji wake kusajiliwa kwa ramani ya upimaji yenye namba za usajili 99770.

Kampuni ya DATACOM HOLDINGS LIMITED imeingia mkataba wa mauziano ya viwanja tajwa na kampuni ya kigeni ya ATLAS BRICKS CO. LTD ya S.L.P 80154 Dar Es Salaam yenye **Certificate of Incentives** yenye namba 02248146 iliyotolewa na ofisi yako tarehe 19 Februari 2021.

Hivyo, tunawasilisha kwako taarifa hii, ili kuwezesha taratibu za ofisi yako za kuhuisha **Certificate of Incentives** ya ATLAS BRICKS CO. LTD ili kuruhusu taratibu za kisheria za umilikishaji wa viwanja tajwa kuendelea.

Nakutakia kazi njema.


M.N Kichumu
Kny: MKURUGENZI MTENDAJI(W)
CHALINZE

Nakala

1. Mkurugenzi Mtendaji

S.L.P 65

CHALINZE

Aione kwenye jalada

2. Kamishna wa Ardhi Msaidizi

Mkoa wa Pwani

S.L.P 9230

DAR ES SALAAM

3. Mkurugenzi

ATLAS BRICKS CO. LTD

S.L.P 80154

DAR ES SALAAM

4. Mkurugenzi

DATAKOM HOLDINGS LIMITED

S.L.P 67468

DAR ES SALAAM

DCG/0405/21/TZ

05th May 2021

MKURUGENZI MTENDAJI (W)
HALMASHAURI YA WILAYA CHALINZE
P.O. Box 65, Chalinze
PWANI, Tanzania

YAH: UTHIBITISHO WA TARATIBU ZA UMILIKISHAJI MPYA WA ARDHI
SOMO: VIWANJA NAMBA 18, 19, 20, 21, 22, 23, 24, 25, 26, 27, 28, 29, 30,
31, 32 NA 33, KITALU "D" – PINGO CHALINZE URBAN

Tafadhali rejea kichwa cha habari hapo juu na kumbukumbu za barua zifuatazo: DCG/0303/20/TZ ya 12/5/2020, iliyojibiwa kwa barua yenye Kumb. Na.HWC/L.20/3/VOL.III/105 ya tarehe 22/5/2020.

Nyaraka zote zilizoombwa katika barua tajwa hapo juu; ziliwakilishwa kwa wakati isipokuwa **Cheti cha Uwekezaji (Certificate of Inventive)** Kutoka Kituo cha Uwekezaji Tanzania (Tanzania Investment Center- TIC).

Hivyo basi, **DATAKOM (Muuzaji)** inaomba ofisi yako kutoa uthibitisho wa taarifa sahihi kwenda Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC) kuhusu taratibu za umilikishwaji mpya wa ardhi katika viwanja tajwa hufanyike kwa jina lifuatalo: **ATLAS BRICKS Co. LIMITED (Mnunuzi)** yenye usajili wa kampuni No.: **140718343**.

Tunatanguliza shukrani zetu za dhati; maombi yetu yakubalike, ili kwa pamoja tujenga nchi ya viwanda.

Asante tunaomba kuwakilisha.


.....
LeoPold RWEYEMAMU
Mkurugenzi

Nakala kwa:
MKURUGENZI
ATLAS BRICKS Co. LTD
S.L.P 80154
Dar Es Salaam, Tanzania – (Kwa Taarifa na Ufuatiliaji)

✓ MKURUGENZI
TANZANIA INVESTMENT CENTRE (TIC)
P.O. Box 938
11477, Dar es Salaam – (Kwa Taarifa)

KAMISHINA WA ARDHI
MKOA WA PWANI
P.O. Box 9230,
11477, Dar es Salaam, Tanzania – (Kwa Taarifa)



49/9 DataCom Campus
Bunju Beach Road, Bunju
P.O. Box 67468
Dar es Salaam, Tanzania
t:+255754262702
t:+255658321090
e:info@datacom.co.tz
w:www.datacom.co.tz

